JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Shule ya Sekondari Maneromango
S.L.P 28085
Kisarawe
Tarehe ……
maneromangosec@gmail.com

Mob; Mkuu wa shule – 0713373594
Makamu M/Shule – 0714561020

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……
S.L.P ……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE MKOA WA PWANI MWAKA 2021/2022

Nafurahi kukujulisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha tano mwaka 2021/2022 Napenda kuchukuwa nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha hapa shuleni na bila shaka utapenda kuishi na kunufaika na mambo yanayoendeshwa hapa shuleni. Nategemea kwamba muda wote utakapokuwa katika shule hii utashirikiana na wanafunzi wenzako, walimu na wafanyakazi wasio walimu katika kutoa mchango wako wa mawazo na vitendo ili kuleta na kudumisha sifa nzuri na maendeleo ya shule hii.
Shule hii ya Maneromango ipo katika Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, umbali wa kilometa 65 kutoka Dar es salaam. Unapokuja Maneromango itabidi upande mabasi yanayokwenda Msanga au Maneromango. Mabasi yanaanzia safari katika kituo cha Pugu –kigogo sokoni jijini Dar es Salaam nauli shilingi 4,000/=

Pamoja na barua hii naambatanisha taarifa zifuatazo:

- **(a)** Fomu ya kujiunga na shule (Joining Instructions) – hakikisha unaisoma neno kwa neno.
- **(b)** Fomu ya taarifa za mwanafunzi(MSS.K5. A) na fomu ya uthibitisho(MSS.K5.B). Fomu hizi zitatakiwa kujazwa na mzazi/mlezi na utazileta shuleni na kuzikabidhi siku ya kuripoti.
- **(c)** Fomu ya uchunguzi wa afya (MSS.K5.).

Mwisho, nakufahamisha kuwa muhula wa masomo unaanza tarehe …/07/2021 hivyo,unatakiwa **ufike shuleni** kuanzia tarehe …/07/2021 na mwisho ni tarehe …/07/2021. Fika **kabla ya saa kumi na mbili (12:00) jioni**. Mara ufikapo shuleni utapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atakupeleka ofisi ya malezi ambapo utasajiliwa. Kama utachelewa kuripoti nitaiarifu Wizara (TAMISEMI) ili waweze kuchagua mwanafunzi mwingine wa kuchukua nafasi yako. Nakutakia safari njema.

Karibu Maneromango.

……..
PILI MWAJIRI
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO

FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)

Soma maelezo haya kwa uangalifu na umakini na uyatekeleze;

1. VIFAA MUHIMU

(a) Mahitaji ya darasani:- kalamu, kasha la vyombo vya hisabati, daftari mbili (2) kwa kila Somo. Daftari zinazotakiwa ni "Quire" 3 au "Quire" 4.
(b) Godoro lenye upana wa futi 2.5
(c) Shuka mbili (rangi ya bluu bahari kwa wavulana na rangi ya pinki kwa wasichana), blanketi, mto, foronya, taulo na chandarua rangi nyeupe.
(d) Scientific calculator (kwa masomo ya science na hisabati).
(e) Shule ina upungufu wa vitabu kwa hiyo unashauriwa uwe na vitabu Binafsi kwa masomo yako.
(f) "Laboratory coat," 'stop watch'na 'thermometer' (kwa wanafunzi wa Physics na Chemistry).
(g) Sanduku la bati na kufuli lake kwa usalama wa vifaa vyake

NB: Orodha ya vitabu kwa masomo yenye upungufu imeambatanishwa.

2. SARE

Unatakiwa uje na sare ya shule kama ifuatavyo na **uwe na idadi ya kutosha** kubadilisha kuanzia mbili na kuendelea. Sababu yoyote ya kutovaa sare haikubaliki;

i. Suruali 2 kwa wavulana zenye marinda mawili na sketi 2 ndefu kwa wasichana mshono wa rindaboxi, rangi bluu nyeusi (Dark blue).SAMPLE ZINAPATIKANA SHULENI .
ii. T-shirt ya shule yenye nembo ya shule.Sample zinapatikana shuleni.
iii. Sweta moja rangi ya suruali/sketi.
iv. Shati 2 nyeupe za mikono mirefu.
v. Soksi jozi 2 nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.
vi. Viatu vyeusi vya Kamba visigino vifupi.
vii. Sare ya kushindia(shamba dress)Sketi nyeusi kwa wasichana na T-sheti nyekundu, suruali nyeusi kwa wavulana na T-sheti ya kijani kwa ajili ya kushindia, (T-sheti zote ni form six zisizo na maandishi)
viii. Traki suti dark blue zisizobana na isiyo na maandishi wala picha.
ix. Sare ya michezo jezi ya timu ya taifa rangi ya bluu
x. Raba za michezo jozi 1.

NB: 1. Zingatia rangi na maelekezo yote ya sare za shule, nguo za nyumbani haziruhusiwi

3.VYOMBO VYA CHAKULA;

Nunua vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe pamoja na kijiko.

ANGALIZO; Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalumu (special diet) kwa wanafunzi wenye matatizo.

4. (A)

MALIPO SHULENI	KIDATO CHA TANO	KIDATO CHA SITA
i) Karo (ada)	70,000	70,000
iv) Ukarabati wa Samani	15,000	15,000
v) Kitambulisho na Picha	6,000	-
vi) Tahadhari (caution money)	5,000	5,000
vii) Taaluma	20,000	20,000
viii)Mitihani endelevu ya kujipima	20,000	20,000
ix) Ulinzi/Wapishi na Mkutubi	30,000	30,000
x) Matibabu	10,000	10,000
JUMLA	176,000	170,000

ANGALIZO: Ada ya mtihani wa Mock na NECTA italipwa kulingana na maelekezo ya viwango vya wakati huo kutoka mamlaka husika**.**

(B) UTARATIBU WA KULIPIA;

Shule haipokei **fedha tasilimu** au hundi kutoka kwa wazazi / walezi wa wanafunzi na badala yake malipo yote yaliyoanishwa kwenye jedwali hapo juu yalipwe kupitia **BENKI** (isipokuwa fedha zilizoainishwa nje ya jedwali)**.** Malipo yanatakiwa yatumwe shuleni kupitia **Benki ya NMB** (National Microfinance Bank) kwenye tawi lililopo karibu na wewe kabla ya kuja shuleni kwa kufuata utaratibu ufuatao;

- Onana na karani wa Benki na umpe taarifa ya kutaka kutuma ada ya shule. Yeye atakupa maelekezo ya kujaza fomu (Bank Pay in Slip nakala 3).
- Utajaza "Bank Pay in Slip" nakala tatu. Nakala moja itabaki Benki, nyingine kwa mzazi/mlezi na nakala ya tatu utaileta shuleni , na utapewa stakabadhi kwa malipo yote.
- Fedha zote hizi zitumwe kwenye Akaunti ya shule, **Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi anayelipiwa kwenye karatasi ya malipo** kama ifuatavyo:-

  Jina la Akaunti: **MANEROMANGO SECONDARY SCHOOL**

  Namba ya Akaunti: **21401100004**

ANGALIZO: Nakala ya 'slip' ya benki utakayoileta shuleni, hakikisha umeiandika kwa nyuma mchanganuo wa fedha uliyoilipa kwa kila mchango. Pesa zinazotakiwa kulipiwa Benki ni zile za kwenye **jedwali tu**

5. KARATASI KWA AJILI YA MAZOEZI NA MAJARIBIO:-

Unatakiwa kuleta karatasi kwa kila mwaka wa masomo kama ifuatavyo:

1. Photocopy paper (A4 size) ulete ream moja kwa kila mwaka
2. "Ruled paper" (karatasi za mistari) ulete moja kwa kila mwaka

6. **USAFI:** Unatakiwa kushiriki kazi zote za usafi na utunzaji mazingira kwa kadiri ya kanuni na taratibu za shule. Hivyo unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo:-

i. Ndoo ndogo 2.
ii. Fyekeo 1 (Kwanja)
iii. Soft bloom 1 (fagio refu laini la ndani) kwa wasichana
iv Fagio gumu (hard bloom) 1 kwa wavulana
iv. Jembe lenye mpini 1
v. Squizer (rubber squeezer)

NB: Vifaa vyote vinapatikana pia shuleni (Duka la shule) kuepuka usumbufu wa kusafiri navyo. (Kununua shuleni ni hiyari, mzazi/mlezi unaweza kununua hukohuko uliko na ukaja navyo)

7. MAWASILIANO:-

1. Mwanafunzi hatakiwi kuja na simu shuleni, mzazi au mlezi hakikisha mwanao haji na simu shuleni. Iwapo atakamatwa na simu shuleni atanyang'anywa na hatarudishiwa tena. Pia atapewa adhabu kali.
2. Mawasiliano na mzazi au mlezi yatafanyika kwa utaratibu uliowekwa na shule.
3. Unatakiwa kuripoti ofisi ya malezi kila mara unapotoka likizo kuja shuleni.

ANGALIZO:

1. Shule ya Maneromango ni ya bweni kwa kidato cha tano hivyo mwanafunzi haruhusiwi kurudi nyumbani au kutoka nje ya shule hadi shule itakapofungwa kwa ajili ya likizo.(ISIPOKUWA KWA KIBALI AU RUHUSA MAALUM). Kama itagundulika umetoka nje ya shule bila kibali / bila kuvaa sare ya shule utapewa adhabu kali.
2. Mwanafunzi hurusiwi kukaa na pesa Zaidi ya shilingi elfu 5,000/= ndani ya bweni, Pesa Zaidi ya elfu 5,000/= ikabidhi kwa muhasibu wa shule.

3. MZAZI AU MLEZI HURUHUSIWI KUMWONA MWANAFUNZI SHULENI BILA RUHUSA KUTOKA UTAWALA:

Likitokea hili mwanao atapewa adhabu kali. Siku za kuwaona wanafunzi ni kila ijumaa ya mwisho wa mwezi muda wa kazi ili uweze kujua maendeleo ya mwanao kitaaluma.

4. DHARURA:

Dharura yoyote itakayompata mwanafunzi kumtaka arudi nyumbani **akiwa katika hali yoyote ile** atakayo kuwa nayo mfano:- ugonjwa, kusimamishwa masomo, n.k. gharama zote zitagharamiwa na mzazi au mlezi. Shule itatoa taarifa tu kwa mzazi / mlezi.

5. Mwanafunzi **lazima** aje na cheti cha kuzaliwa na result slip. (Halisi na kivuli)

ORODHA YA VITABU

SOMO	JINA LA KITABU	MWANDISHI / MTUNZI
FIZIKIA	• Principals Physics	S. CHAND

	• UNIVERSITY Physics • College Physics	R. ZEMAN SKY F. MILLER
KEMIA	• Advanced inorganic Chemistry I and II • Organic Chemistry part A • Organic Chemistry part B • Conceptual Chemistry volume I, II, III. • A level Chemistry • Physical Chemistry for Advanced level 1st year undergraduate students.	P.M GUIRE M.G NKUNYA P.M GUIRE M.H NKUNYA CHAND'S E.N RAMSEDEN MZUMBE BOOK PROJECT I B.A. MILIGO, L.L.MKANYULA and ABS MKWIZU
ADV. MATH'S	• Pure Mathematics 1 & II • Advance Mathematics Review • Advanced Mathematics Core Series • Pure Mathematics • Understanding Mathematics • Advanced Mathematics	BACKHOUSE MZUM BE PROJECT BASTOCKS BASTOCKS SADRAL TRANTER
BASIC APPLIED MATHS.	• Basic Applied Mathematics Form V • Basic Applied Mathematics Form VI • Basic and Applied Mathematics	S. I. SILLEM 1st Ed. 2014 S. I. SILLEM LUGANO MWANGINDE and RESPICIUS KIIZA
GENERAL STUDIES	• Contemporary Approach For Advanced Level Form 5 & 6 • General Studies For Advanced Level Certificates Form Five	NYAMBARI NYANGWINE RICHARD MBALASE
KISWAHILI	• Sarufi muundo ya Kiswahili(SAMIKISA) • Fasihi na Sarufi Sekondari na Vyuo • Riwaya Vuta n'kuvute, Mfadhili, usiku utakapokwisha, kwenye ukingo wa thim, kimbunga, chungu tamu.	Mkwera
HISTORY	• Major Events in African History • Major Events in te World History • Mastering Modern World Africa • History for Secondary School	Gervas M. Zombwe Norman Lowell TIE
ENGLISH LANGUAGE	• English for Advance Level, Phonology, Stylistics • English for Advance level Phonology, Stylistics & Semantics • Advance level Literature Form 5 & 6	M. Kadeghe M. Kadeghe

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule**.**
7. Kufuga ndevu
8. Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya dawa za kulevya
9. Uvutaji sigara
10. **U**asherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
11. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
12. . Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
16. Kudharau Bendera ya Taifa
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
18. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

KUMBUKA: Kitu chochote kilichokatazwa ukikutwa nacho hutorudishiwa na utapata adhabu kali mfano simu, pesa Zaidi ya elfu 5 Bwenini, vipodozi, nguo n,k

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO

FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI **MSS.K5.A**

1. Jina lako kamili……

2. Kidato ulichojiunga hapa shuleni……..mchepuo……

3. Jina la mzazi/mlezi…….
Anuani yake…….Simu ya Ofisini…….simu ya mkononi…….
Kazi yake…….

4. Mahali ulipozaliwa
(i) Mkoa…… Wilaya …… Kata……
(ii) Tarafa…… Kijiji cha ……..
(iii) Tarehe ya kuzaliwa …….

5. Mahali unapoishi sasa……
Anuani yako……..
Namba za simu……

6. Dini/dhehebu lako…….

7. Unaishi na Baba tu/mama tu/wazazi wote/mlezi…….

8. 1. Jina la shule za msingi ulizosoma……
(i) Shule ya msingi ya ……Anuani…….
(ii) Shule ya msingi ya ……Anuani……..
2. Jina la shule za sekondari ulizosoma…….
(a) Shule ya sekondari uliyoanzia…….Anuani…….
(b) Shule ya sekondari uliyomalizia……Anuani……..

9. Michezo unayocheza
(a)…….
(b) ……

10. Vyama vya kujifunza ambavyo wewe unapenda kuwa mwanachama:
Scout, Fema, Wapinga Rushwa(PPCB), YUNA, Mali Hai,Ant Aids, School Magazine na Mazingira.
(a)……..
(b)……
(c)……

11. Je unao ulemavu wowote? (Ndiyo / Hapana)
Kama Ndiyo taja aina ya ulemavu……..

N.B: Mazingira ya shule si rafiki kwa watoto wenye ulemavu.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO

FOMU YA UTHIBITISHO **MSS.K5.B**

Fomu hii ijazwe na mzazi au mlezi wa mwanafunzi katika sehemu zake na irudishwe shuleni ikiwa imeambatanishwa na picha ya mzazi/mlezi. Shule itatoa taarifa kwa mzazi / mlezi ambaye picha yake na maelezo yake yataonekana katika fomu hii.

Mimi……mzazi/mlezi wa mtoto wangu ……nimeona, nimeelewa na nimekubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari ya Maneromango.

Nitampa mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na walimu wa shule ya Maneromango katika kumlea vizuri mtoto wangu ili aweze kusoma na kuelewa na hatimaye aweze kufanya mitihani yote ya ndani shuleni na ya Taifa kwa mujibu wa ratiba.

Saini ya mzazi/mlezi…….
Anuani ya mzazi
……..
……
Simu…….

TAMKO LA MZAZI/MLEZI:

Mimi…… mzazi/mlezi wa mwanafunzi……wa kidato cha tano.
Nakiri kwamba yaliyoandikwa hapo juu kwenye fomu zote mbili (MSS.K5.A na MSS.K5.B) ni sahihi.

SAINI YA MZAZI/MLEZI

…….
Tarehe……..

Picha ya mzazi/mlezi

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO

FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA **MSS.K5.**

(Request for Medical Examination)

This form is to be completed by a Medical Officer.

Name of Student:…… **Age:** …….. **Sex:** ……

The above named has been examined in respect of:

(a) STOOL ……

(b) URINE ..……

(c) CHEST …….....

(d) BLOOD …….

(e) EYES ……

(f) EARS ……

(g) HEART ……..

(h) STOMACH ULCERS ……...

(i) OTHERS …….

I am satisfied / not satisfied that the above named Student is physically and mentally fit to pursue further studies in Secondary School.

…… **…….**

SIGNATURE(and official stamp) **DATE**

…… **…….**

DESIGNATION **STATION**